

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUSIMAMISHWA KWA HUDUMA YA MATANGAZO YA TELEVISHENI  
KWA NJIA YA SATELAITI NA KAMPUNI YA GTV TANZANIA LIMITED**

Mnamo siku ya Ijumaa ya tarehe 30 Januari 2009, Kampuni ya GTV (Tanzania) Limited ilisimamisha kutoa matangazo yake ya televisheni kwa njia ya satelaiti kwa wateja wake ghafla bila taarifa yeyote ya awali kwa wateja wake. Sababu za kusimamishwa matangazo ya GTV (Tanzania) Limited ni hali mbaya ya uchumi inayoendelea duniani ambapo kampuni ya Gateway Broadcast Services ya Uingereza ambayo ilikuwa inaipatia GTV (Tanzania) Limited Maudhui (content) ilifilisika baada ya kuathirika na hali hiyo mbaya ya kiuchumi.

Mnamo tarehe 2 Februari Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ambayo pamoja na majukumu yake mengine ni kulinda maslahi na haki za wateja, iliwaita GTV katika ofisi zake ili kutoa taarifa ya yaliyotokea na kujadili haki za wateja wake. Kumekuwa na mikutano mingine kati ya Mamlaka ya Mawasiliano na GTV (Tanzania) ukiwemo wa tarehe 10 February 2009 katika kufuatilia haki za wateja.

Tunapenda kutoa maelezo yafuatayo kwa umma;

1. GTV (Tanzania) Limited inamilikiwa kwa mujibu wa matakwa ya Sheria na kanuni kwa asilimia 51 Mtanzania na GTV Holdings Limited (Mauritius) yenye kumiliki asilimia 49;
2. Kampuni ya GTV Tanzania Limited ilipewa leseni na Mamlaka ya Mawasiliano tarehe 12 Septemba 2007 ya kutoa huduma za matangazo ya televisheni ya kulipia kwa njia ya satelaiti Tanzania Bara;
3. GTV (Tanzania) Limited ilisimamisha huduma zake tarehe 30 Januari 2009, kama ilivyoelezwa hapo juu;
4. Wakati inasimamisha huduma zake, GTV (Tanzania) Limited ilikuwa na wafanyakazi 35, maajenti 40 na wateja 20,000;

5. Menejimenti ya GTV (Tanzania) Limited imeiarifu Mamlaka ya Mawasiliano kuwa Mfilisi anatarajiwa kuteuliwa na Mahakama hivi karibuni ambaye atashughulikia masuala yote ya wadeni wa GTV (Tanzania) Limited;
6. Utoaji leseni kwa GTV (Tanzania) Limited ulizingatia sharti la kampuni hiyo kuweka dhamana kuhakikisha ufanisi wa huduma zake kwa jamii.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inapenda kuwathibitishia wateja wote wa GTV (Tanzania) Limited kuwa haki zao zitalindwa kwa mujibu wa Kanuni na sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

Imetolewa na:

**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**